



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**TAARIFA YA WAZIRI WA NCHI AFISI YA MAKAMU WA PILI
WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI
MHE. DKT. KHALID SALUM MOHAMED JUU YA
MUELEKEO WA KIMBUNGA "JOBÓ"
NA HATUA ZA TAHADHARI ZINAZOPASWA KUCHUKULIWA**

Ndugu Wananchi;

Kama tulivyosikia taarifa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kuwa nchi yetu inaweza kukumbwa na Kimbunga kinachojulikana kwa jina la 'Jobo'. Kwa mujibu wa taarifa hiyo kimbunga Jobo kimeendelea kusogea kuelekea maeneo ya pwani ya nchi yetu yakiwemo maeneo ya Lindi, Mtwara na kisiwa cha Mafia kikitokea upande wa kisiwa cha Madagascar. Kimbunga hicho kinaweza kupelekea kutokea kwa mvua kubwa na upepo mkali unaoweza kufikia kasi ya kilomita 60 kwa saa.

Ndugu wananchi;

Taarifa ya Mamlaka hiyo pia imeeleza kuwa athari za kimbunga hicho zinategemewa kuanza kuonekana kuanzia majira ya saa 6 mchana wa leo tarehe 24 Aprili, 2021 katika maeneo ya pwani ya nchi yetu na kinatarajiwa kuingia maeneo ya nchi kavu kesho Jumapili tarehe 25 Aprili, 2021. Miongoni mwa maeneo yanayoweza kuathirika moja kwa moja kutokana na Kimbunga

hicho yameelezwa kuwa ni pamoja na kisiwa cha Unguja na Pemba.

Ndugu wananchi

Ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na kimbunga hicho Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuchukua hatua zifuatazo:-

1. Kusitisha shughuli zote za baharini zikiwemo za uvuvi, safari za meli na vyombo vyengine vya usafiri baharini kuanzia leo tarehe 24 Aprili, 2021 saa tatu (3:00) asubuhi hadi pale taarifa nyengine zitakapotolewa na Mamlaka zinazohusika.
2. Serikali inawataka wananchi wanaoishi katika majengo ambayo uimara wake hauko vizuri hasa wa maeneo ya pwani na Mji Mkongwe na wale waliokaribu na miti mikubwa kuhama katika majengo hayo na badala yake kuhamia majengo yaliyosalama ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.
3. Wananchi wanaokaa maeneo hatarishi yenye kutuama maji kama vile Mtumwajeni, Ziwa Maboga, Jangamizini, Chuini wanatakiwa kuchukua tahadhari ili kuepukana na athari zinazoweza kutokea.
4. Wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari na kuzuia watoto kutoshika nyaya za aina yoyote pindi ikitokea nguzo

kuanguka au nyaya kuangukiwa na miti na kuepuka kushika miti au kitu chochote kilichoshikana na nyaya. Aidha, wananchi wanatahadharishwa kutokupita katika madimbwi ya maji yaliyokaribu na nyaya zilizoanguka.

5. Serikali pia imezitaka Kamati zote za kukabiliana na maafa za Shehia na Wilaya, vikosi vya ulinzi na usalama na taasisi zote zinazohusika katika kukabiliana na maafa zikiwemo Shirika la Umeme, Mamlaka ya Maji na Wizara ya Afya kujiweka tayari katika kukabiliana na hali yoyote inayoweza kujitokeza kutokana na kimbunga Jobo.

6. Aidha, Serikali imewataka wananchi wote kwa madhehebu ya dini zao kuendelea kuiombea dua nchi yetu ili kuepukana na athari za kimbunga hiki.

Ndugu wananchi;

Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inaendelea kufuatilia mwenendo wa kimbunga hiki na itatoa taarifa kwa wananchi kadri ya hali inavyoendelea. Hivyo, niwaombe wananchi waendeleo kufuatilia taarifa zinazotolewa na Serikali na Mamlaka ya Hali ya Hewa kupitia vyombo mbali mbali vya habari na kuchukua hatua stahiki ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushie janga hili na mengine katika nchi yetu na nchi nyengine duniani.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza

.....

DKT. KHALID S. MOHAMED

WAZIRI WA NCHI

AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR